**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY (TPHPA)**

TPHPA
TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA

## TAMKO KUHUSU USALAMA NA UBORA WA MAHINDI YA TANZANIA KATIKA MASOKO YA KIKANDA NA KIMATAIFA

07/02/2025, Arusha- Tanzania.

Tanzania ni mzalishaji mkubwa namba mbili (2) wa zao la Mahindi barani Afrika. Katika msimu wa 2023/24, Tanzania ilizalisha jumla ya tani milioni 11.7 ikiwa ni ongezeko la tani milioni 6.4 ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2022/23. Tanzania husafirisha takribani tani nusu milioni kila mwaka kwenda katika Ukanda wa nchi za Afrika Mashariki na za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Mchango wa Mahindi ya Tanzania katika kuimarisha usalama wa chakula kikanda ni mkubwa hasa katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula salama na cha kutosha kwa walaji.

Mahindi yanayosafirishwa kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi ni salama na yanazingatia matakwa yote ya afya mimea na viwango vya ubora ikiwemo:-

1. Kufanya "survey" kila mara katika maeneo yote ya uzalishaji Mahindi nchini ili kutambua magonjwa muhimu kama vile UVIMA (Maize Lethal Necrosis Disease – MLND) na kuchukua hatua madhubuti za kuyatokomeza.
2. Kuchukua sampuli na kupima uwepo wa virusi vya MLN kwenye mbegu zote za Mahindi zinazoingia nchini kutoka nchi zinazojulikana kwamba zimeathiriwa na ugonjwa huu na kuchukua hatua muafaka.
3. Kuchukua sampuli katika Mahindi yaliyohifadhiwa katika bohari zote nchini Tanzania, ikiwemo zile za (National Food Reserve Agency – NFRA), na kupima uwepo wa virusi vya MLN kabla ya kuidhinisha kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

4. Kuelimisha wakulima kupitia machapisho, warsha, vipindi vya redio na mitandao ya kijamii.
5. Kukagua mashamba ya mbegu wakati wa uzalishaji na kuyathibitisha (certification) kabla ya kuanza kusambaza na kuuza mbegu.
6. Kuchukua sampuli na kupima sumu kuvu, masalia ya Viuatilifu, unyevu sahihi na uwepo wa mabadiliko ya kijenetiki (Genetically Modified Organism – GMO) kwenye kila shehena ya mizigo inayosafirishwa nje ya nchi.
7. Kufanya ukaguzi na upimaji sampuli wa pamoja na mataifa washirika wetu wa kibiashara kama vile ilivyofanyika hivi karibuni na Wataalam toka nchi za Zambia na Malawi.

Katika kuthibitisha hilo, Tanzania haijawahi kupata taarifa ya malalamiko ya kutokidhi viwango **(Notification of non-compliance)** kwa shehena za Mahindi yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi.

Tanzania itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha biashara salama kwa washirika wake wa kibiashara Kikanda na Kimataifa na tunapenda kuzialika nchi zenye nia ya kununua Mahindi kutoka Tanzania kuwasiliana na TPHPA ili kuweka utaratibu wa namna ya kukidhi masharti na matakwa ya nchi mwagizaji.

Imetolewa na,

Prof. Joseph C. Ndunguru
**MKURUGENZI MKUU**

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY
P.O. Box 3024, Tel.: +255 27 297 0487
ARUSHA - TANZANIA